**BUNGE LA TANZANIA**

---

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (FUNGU 38, 39, 57) KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

# YALIYOMO

**ORODHA YA MAJEDWALI ........................................................................ iii**

**ORODHA YA GRAFU ................................................................................ iv**

**ORODHA YA CHATI ................................................................................. v**

**1.0 UTANGULIZI ......................................................................................... 1**

**2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO .......................................... 2**

2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa……..3

2.2 Matokeo ya Ukaguzi……………………………………………..5

2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022…………….6

**3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 .................................................................... 8**

3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022…………………….8

3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa............ 8

Mapato ........................................................................ 8

3.1.2 Upatikanaji wa Fedha Kutoka Hazina ....................... 12

3.2 Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati……………..16

**4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ......................... 17**

4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023……………………………………17

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023…………………………………………………...18
4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi…………………….20
**5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI ............................................... 22**
5.1 Maoni ya Kamati…………………………………………………...22
5.2 Ushauri wa Kamati……………………………………………….23
**6.0 HITIMISHO........................................................................................ 26**
***KIAMBATISHO NA. 1 ........................................................................... i***

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali 1:** Mchanganuo wa Makadirio na Makusanyo ya Mapato 10

**Jedwali 2:** Ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa miongoni mwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57 .............. 13

**Jedwali 3:** Ulinganisho wa fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na zilizopokelewa miongoni mwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57 .......................................................................... 13

**Jedwali 4:** Mchanganuo wa Makadirio ya mapato ............................ 18

## ORODHA YA GRAFU

**Grafu 1:** Ulinganisho wa lengo na Makusanyo halisi ya Mapato....... 10

**Grafu 2:** Ulinganisho wa Makusanyo 2020/2021 na 2021/2022........... 11

## ORODHA YA CHATI

**Chati 1:** Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo 2022/202319

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (FUNGU 38, 39, 57) KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) na Kifungu cha 7 (1) (a), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni hizo, kabla ya taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na JKT, kujadiliwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Uchambuzi huo ulifanyika tarehe 29 Machi, 2022 baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii kama ilivyoelekeza Kanuni ya 117 (1) hadi 117 (2) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuweka bayana mawanda ya Taarifa hii, nitangulie kulikumbusha Bunge hili kuwa Wizara ya Ulinzi na JKT inajumuisha Mafungu Matatu (3) ya Kibajeti yafuatayo: -

i) Fungu 38- Ngome;
ii) Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa; na
iii) Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Wizara).

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu kuu nne (4) zifuatazo: -

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na
iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Kuendeleza utafiti katika Shirika la NYUMBU, kuendeleza uzalishaji katika shirika la MZINGA. Aidha, kamati pia ilitembelea mradi wa ukarabati miundombinu ya umwagiliaji Chita pamoja na ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi Kikombo. Miradi hiyo ipo Mikoa ya Pwani, Morogoro na Dodoma mtawalia.

Maeneo yaliyotembelewa ni sehemu ya miradi inayotekelezwa na Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Taarifa hii inaeleza mambo makuu mawili:

a) Muhtasari wa maelezo ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022; na

b) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la sehemu hii ni kuliwezesha Bunge kufuatilia hali ya utekelezaji na upatikanaji wa Fedha ilizo ziidhinisha na kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

## 2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika**, maelezo kuhusu maeneo yaliyokaguliwa ni kama ifuatavyo:-

### 2.1.1 Kuendeleza utafiti katika Shirika la NYUMBU-Kibaha

Shirika la NYUMBU lilitengewa kiasi cha **Shilingi bilioni 9** kwa ajili ya kuendeleza utafiti katika Shirika hilo. Hadi Kamati inafanya ziara Shirika hilo lilikuwa limepokea kiasi cha **Shilingi 8, 952,541,837.25** ikiwa ni zaidi ya asilimia 97 ya fedha iliyotengwa. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa fedha hizo zimetumika katika ununuzi wa mashine na mitambo mipya kwa ajili ya uzalishaji wa Shirika.

### 2.1.2 Uendelezaji wa Uzalishaji katika Shirika la MZINGA

Kamati ilipata wasaa wa kutembelea na kukagua utekelezaji wa bajeti katika Shirika la MZINGA Mkoani Morogoro**.** Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali ilitenga kiasi cha **Shilingi 5,500,000,000** kwa ajili ya uendelezaji wa uzalishaji katika Shirika la MZINGA. Hadi Mwezi Machi, 2022 Serikali ilikuwa imetoa fedha kiasi cha Shilingi **5,465,210,622.68** ikiwa ni sawa na asilimia 98 ya bajeti iliyopangwa**.**

### 2.1.3 Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Chita

**Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) linatekeleza mradi wa kilimo cha mpunga kwenye shamba lake lenye ekari 12,000 lililopo eneo la Chita, Halmashauri ya Mlimba. Katika kutekeleza mradi huo Jeshi limeanza na kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji sambamba na mpango wa kuanza kulima ekari 2500. Hadi Kamati inatembelea mradi huu JKT imetumia kiasi cha Shilingi 5.6 bilioni kwa ajili ya kuimarisha miundombinu. Aidha, ili mradi wa miundombinu ukamilike inahitajika kiasi cha Shilingi 3.3 bilioni. Vilevile Kamati ilielezwa kuwa inahitajika kiasi cha Shilingi 6.2 bilioni ili kusawazisha ardhi (Levelling) kwa ekari zote 2,500. Hii inapelekea kuwa na upungufu wa jumla ya Shilingi 9.5 bilioni.

Kamati ilielezwa kuwa ikiwa mradi huu utakamilika na kuanza uzalishaji Utasaidia kupata

uhakika wa usalama wa chakula kwa Jeshi na Taifa kwa ujumla. Mathalani, kwa ekari 2,500 zinaweza kuingiza sokoni magunia ya mpunga yenye ujazo wa kilo 100 yapatayo 62,500 kwa msimu mmoja.

### 2.1.4 Ujenzi wa Jengo kuu la Ulinzi wa Taifa- Kikombo

**Mheshimiwa spika,** Jeshi la Wananchi wa Tanzania linatekeleza mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi katika eneo la Kikombo Mkoani Dodoma. Ujenzi wa mradi huo ulianza Mwezi Machi, 2020 na unatarajiwa kukamilika Mwezi Oktoba, 2022.

**Mheshimiwa Spika** Mradi huu unajengwa kwa kutumia *Force Account* kwa kiasi cha Shilingi 58 bilioni. Ikiwa ujenzi huo usingejengwa kwa F*orce Account* ungetumia kiasi cha Shilingi 127 bilioni. Hivyo utaratibu huo umeokoa kiasi cha Shilingi 69 bilioni. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 41.5

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika**, baada ya muhtasari wa miradi ya maendeleo iliyokaguliwa, sasa naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya uchambuzi wa miradi hiyo kwa kutaja yafuatayo:

i) Utekelezaji wa majukumu ya Mashirika ya NYUMBU na MZINGA unaridhisha mbali ya kwamba yanakabiliwa na changamoto mbalimbali. Aidha, ushauri wa Kamati kuhusu changamoto hizo umetolewa kikamilifu kwa Mamlaka husika.

ii) Kamati iliridhishwa na uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Chita. Mradi huu wa kilimo cha umwagiliaji ni muhimu kwa usalama wa chakula kwa Taifa; pamoja na umuhimu wake, Kamati ilielezwa kuwa unakabiliwa na changamoto zifuatazo;-

a) Ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji pamoja na gharama nyingine za kilimo; na

b) Uhaba za wa zana na mitambo ya kisasa kwa ajili ya kuhudumia shamba.

## 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

i) NYUMBU ni Shirika la Kimkakati na katika kuhakikisha Shirika hilo linakuwa kubwa na kufikia malengo ya uanzishwaji wake tayari lina Mpango wa Maendeleo wa Miaka Kumi (2020/2021-2029/30) ambao ikiwa utatekelezwa kwa ukamilifu, ni dhahiri kuwa Shirika litatekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ni rai ya kamati kuwa Serikali itasimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa mpango huo.

ii) MZINGA ni Shirika la kimkakati na kutokana na umuhimu wake ni rai ya Kamati kwamba Serikali itoe kipaumbele katika kutatua changamoto zinazokabili Shirika hilo sambamba na kuliongezea bajeti ya maendeleo mwaka hadi mwaka kwa

kuzingatia mahitaji na kipaumbele cha Shirika hilo.

iii) Mradi wa kilimo Chita ni wa kimkakati na unalihakikishia Taifa chakula kwa mwaka mzima kwa kuwa ni mradi wa umwagiliaji. Dunia sasa inakabiliwa na changamoto ya Mabadiliko ya Tabianchi ambayo husababisha ukame na hivyo kutishia usalama wa chakula. Kwa msingi huo kilimo cha umwagiliaji kinatoa uhakika wa chakula kwa asilimia 100. Hivyo, ni matarajio ya Kamati kuwa Serikali italiunga Jeshi mkono kifedha na kimkakati ili liweze kutekeleza mradi huu kwa ekari zote 12,000 kwa manufaa ya Taifa.

iv) Ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi Kikombo kwa utaratibu wa kutumia *Force account* umeokoa zaidi ya Shilingi 69 bilioni. Ikiwa utaratibu huu utatumika kwa uadilifi ni wazi Serikali itaokoa fedha nyingi hasa katika miradi ya majengo ya kimkakati. Ni rai ya Kamati kuwa Taasisi nyingine za Serikali na watumishi watajifunza namna Jeshi lilivyotumia utaratibu huo wa Force Account kwa uadilifu mkubwa na kwa kuzingatia viwango vya ubora vya ujezi.

v) Ni vema Serikali ikaendelea kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili kibajeti miradi ya wizara hii kutokana na umuhimu wake.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, ulilenga kulinganisha Makusanyo ya Mapato na lengo la Makusanyo hayo, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za Matumizi Mengineyo na upatikanaji wa fedha za Maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, kwa mafungu yote Matatu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Januari, 2022 na Machi, 2022 pamoja na majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha uchambuzi huo kama ifuatavyo: -

#### 3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Mapato

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ilikadiria kukusanya Mapato ya jumla ya Shilingi **85,103,000.00** kwa Mafungu yote matatu (3). Makadirio haya yalikuwa

sawa na lengo lililowekwa la Makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa maelezo ya Wizara, hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 kiasi kilichokuwa kimekusanywa kilikuwa **shilingi 87,679,496.06** sawa na **asilimia 103.03** ya lengo la mwaka lililopangwa. Kamati ilibaini kuwa kiasi kilichokusanywa ni ongezeko la **asilimia 15.23** ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambayo yalikuwa **Shilingi 76,085,664.16** sawa na **asilimia 89** ya lengo lililowekwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa Mafungu yote ya Wizara yamechangia ongezeko hilo; ambapo Fungu 38 (Ngome) limekusanya **asilimia 142** ya lengo lililowekwa, Fungu 39 (JKT) limekusanya **asilimia 87** ya makadirio yake na Fungu 57 (Wizara) imekusanya **asilimia 165** ya lengo lililowekwa.


**Mheshimiwa Spika**, vilevile, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila Fungu na kubainisha mchanganuo wa makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 01** na **Grafu Na. 01** hapa chini.

**Jedwali 1: Mchanganuo wa Makadirio na Makusanyo ya Mapato**

| FUNGU | MAKADIRIO | % YA JUMLA YA LENGO | MAKUSANYO | % YA JUMLA YA MAKUSANYO | % YA LENGO LA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 38 - Ngome | 22,000,000.00 | 25.85 | 31,405,466.00 | 35.82 | 142.75 |
| 39 - JKT | 61,903,000.00 | 72.74 | 54,292,000.00 | 61.92 | 87.70 |
| 57 - Wizara | 1,200,000.00 | 1.41 | 1,982,030.06 | 2.26 | 165.17 |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023***


**Grafu 1: Ulinganisho wa lengo na Makusanyo halisi ya Mapato**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023***

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa Makusanyo yaliyopatikana kwa kila Fungu kufikia Mwezi Februari, 2022 na Makusanyo yaliyopatikana katika kipindi kama hicho katika Mwaka 2021 kama inavyoonekana katika **Grafu na 2** hapa chini:-

**Grafu 2: Ulinganisho wa Makusanyo 2020/2021 na 2021/2022**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2020/2021 na 2021/2022***

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kufanya Uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa:-

i) **Makusanyo katika Fungu 38 – Ngome** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 25.85** lakini katika utekelezaji Fungu hilo limechangia kwa **asilimia 142.75** ya kiasi ilichokusanya.

ii) **Makusanyo ya Fungu 39 –JKT** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 72.74**, lakini hali halisi imeonesha kuwa makusanyo ya JKT yamechangia kwa **asimia 87.70** ya kiasi ilichokusanya.

iii) **Makusanyo ya Fungu 57 – Wizara**, yalikusudiwa kuchangia kwa **asilimia 1.41** kwenye mapato yote ya Wizara, lakini hali halisi imeonesha kuwa makusanyo ya Wizara yamechangia kwa **asilimia 165** ya kiasi ilichokusanya.

**Mheshimiwa Spika,** ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na kiasi halisi kilichokusanywa, umeisaidia Kamati kubaini kuwa mwenendo wa makusanyo ni mzuri na Wizara hadi kufikia Februari, 2022 ilikuwa imevuka lengo la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Aidha, Kamati inapongeza Serikali kwa kuweka makadirio kwa uhalisia.

### 3.1.2 Upatikanaji wa Fedha Kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kupokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2021/2022, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara na kiasi cha Fedha kilichotolewa hadi kufikia Mwezi Februari, 2022.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, katika kujiridhisha na uzito uliowekwa wakati wa utoaji wa fedha kutoka Hazina kama uliendana na uzito uliokusudiwa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ililinganisha uwiano wa Bajeti za Mafungu hayo na uwiano wa fedha zilizopokelewa kwa Mafungu hayo . Ulinganisho huo unaonekana katika **Jedwali Na. 02** na **03** hapa chini:-

**Jedwali 2: Ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa miongoni mwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57**

| Fungu | Kiasi cha fedha zilizoidhinishwa | Asilimia ya fedha zilizoidhinishwa Kiuwiano | | Fungu | Kiasi cha fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa kiuwiano |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 38 | 1,812,053,709,000.00 | 76.82 | | 38 | 53,497,934,254.60 | 52.62 | 74.81 |
| 39 | 386,474,955,000.00 | 16.39 | | 39 | 252,006,541,480.88 | 65.21 | 19.77 |
| 57 | 160,166,322,000.00 | 6.79 | | 57 | 69,081,232,049.00 | 43.09 | 5.42 |
| | **2,358,694,986,000.00** | 100.00 | | | **1,274,522,707,784.48** | 54.04 | 100.00 |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023***

**Jedwali 3: Ulinganisho wa fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na zilizopokelewa miongoni mwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57**

| Fungu | Kiasi cha fedha zilizoidhinishwa | Asilimia ya fedha zilizoidhinishwa kiuwiano | | Fungu | Kiasi cha fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa Kiuwiano |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 38 | 32,578,424,000 | 18.45 | | 38 | 28,317,712,000 | 86.9 | 31.94 |
| 39 | 4,000,000,000 | 2.27 | | 39 | 3,272,048,797 | 81.8 | 3.96 |
| 57 | 140,000,000,000 | 79.28 | | 57 | 57,058,481,631.93 | 40.7 | 64.37 |
| | **176,578,424,000** | 100.00 | | | **88,648,242,428.93** | 50.2 | 100.00 |

Kupitia uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

i) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu imepokea Shilingi **1,274,522,707,784.48** sawa na asilimia 54.04 ya fedha zilizoidhinishwa.

ii) Kati ya fedha zilizopokelewa Shilingi **1,185,874,465,355.55** sawa na asilimia 93.04 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **88,648,242,428.93** sawa na asilimia 6.96 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

iii) Kati ya fedha zilizopokelewa, asilimia 74.81 ni kwa ajili ya Fungu 38 (Ngome), asilimia 19.77 ni kwa ajili ya Fungu 39 (JKT) na asilimia 5.42 ni kwa ajili ya Fungu 57 (Wizara).

iv) Kiasi kilichopokelewa na Wizara hii kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni pungufu ya **asilimia 8.20** ikilinganishwa na Fedha zilizotolewa katika kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambapo kwa kipindi kama hicho ilipokea shilingi **95,917,678,289.97** .

v) Kati ya Shilingi **88,648,242,428.93** zilizopokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, asilimia 64.37 ya Fedha hizo ni kwa ajili ya Fungu 57 (Wizara) na asilimia 31.94 ni kwa ajili ya Fungu 38 (Ngome) na asilimia 3.69 ni kwa ajili ya Fungu 39 (JKT).

vi) Fungu 38 (Ngome) limepokea Shilingi **28, 317,212,000.00** sawa na asilimia 86.92 ya Shilingi **Bilioni 32.5** zilizoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo.

vii) Fungu 57 (Wizara) limepokea Shilingi **57,058,481,631.93** sawa na asilimia 40.7 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa Fungu hilo.

viii) Katika Fedha zilizoidhinishwa kwa kila Fungu, Fungu 38 (Ngome) lilipokea asilimia 52.6, Fungu 39

(JKT) lilipokea asilimia 65.21 na Fungu 57- (Wizara) lilipokea asilimia 43.09.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huo unaonesha kuwa Serikali ilizingatia uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti. Kwa mfano, Bunge liliidhinisha bajeti ya Fungu 38 (Ngome) ikiwa ni asilimia 76.82 ya Bajeti ya Wizara na fedha zilizopokelewa na Fungu hilo ni asilimia 52.6 ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia Mwezi Februari, 2022, na Fungu 39 lililidhinishiwa asilimia 16.59 ya bajeti yote ya Wizara na fedha zilizopokelewa na fungu hilo hadi kufikia Februari, 2022 ni asilimia 19.77 ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara kufikia Februari, 2022 na Fungu 51 ilitengewa asilimia 6.7 ya bajeti yote ya Wizara, hadi kufikia Februari 2022 ilikuwa imepokea asilimia 5.4 ya fedha zote zilizopkelewa na Wizara. Kwa mwenendo huu, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuipa uzito stahiki kwa Bajeti ya Ngome, Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mwenendo huo mzuri, Kamati haijaridhishwa na mtiririko wa fedha za maendeleo kwa ajili ya Fungu 57 (Wizara) ambapo hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 Fungu hilo lilikuwa limepokea **asilimia 40** ya fedha iliyotengewa kwa ajili ya maendeleo.

Ni vema Serikali ikatoa fedha hizo za maendeleo kwa mujibu wa ratiba ya utekelezaji wa miradi iliyowekwa ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza.

## 3.2 Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilishauri masuala mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge kuwa, taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya ushauri kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1** cha Taarifa hii.

Mfano wa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 39-JKT kwa mtiririko uliopangwa. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 Fungu 39 lilikuwa limepokea fedha za maendeleo kwa **asilimia 81.8.** ya bajeti iliyotengewa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri huu na kuisisitiza kuendelea na utaratibu huu kwa Mafungu yote.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uzingatiaji mzuri wa ushauri, upo ushauri ambao unahitaji kufanyiwa kazi na Serikali. Mathalani, ushauri kuhusu Serikali kutoa fedha zote zilizotengwa katika Mwaka 2020/2021 kwa ajili ya kukarabati nyumba za makazi ya wanajeshi. Maelezo yaliyotolewa kwenye Kamati yalibainisha kuwa hakuna fedha zilizotolewa na Hazina kwa ajili hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri ambao haujatekelezwa unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### 4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilipitia majukumu makuu ya Wizara na Kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo kulingana na Dira na Dhima ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu sita likiwemo kuliongezea uwezo wa kimedani Jeshi la ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kulipatia vifaa na zana bora,mafunzo na mazoezi, kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumishi wa umma pamoja kuwapa viijana wa kitanzania mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi ili kuwajengea ukakamavu, uzalendo, umoja wa kitaifa na uwezo wa kujitegemea.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa, majukumu yaliyopangwa yatawezesha ufikiaji wa malengo sita (6) ya Wizara hii kwa ufanisi zaidi endapo Serikali itazingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kutoa Fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia mpango kazi wake.

### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu (38, 39 na 57) inategemea kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 87,603,000** Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 2.9 ikilinganishwa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ongezeko hili linatarajiwa kuwa katika Fungu 39- JKT ambapo lengo la makusanyo yake limeongezeka kwa asilimia 4.


**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kuongeza lengo la makadirio kwa Fungu hilo, hususan kwa kuzingatia kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 Fungu 39- JKT lilikuwa limeshakusanya asilimia 87.7 ya makadirio yaliyowekwa katika mwaka wa Fedha 2021/2022. Mchanganuo wa lengo hilo la Makusanyo na Sura ya mchanganuo wake inaonekana katika **Jedwali Na. 04.** na **Chati Na. 03** hapa chini: -

**Jedwali 4: Mchanganuo wa Makadirio ya mapato**

| Fungu | Makadirio | Asilimia ya lengo la Wizara |
|---|---:|---:|
| Fungu 38 - Ngome | 22,000,000.00 | 25 |
| Fungu 39 - JKT | 64,403,000.00 | 74 |
| Fungu 57 - Wizara | 1,200,000.00 | 1 |
| **JUMLA** | **87,603,000.00** | **100** |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023***

**Chati 1: Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo 2022/2023**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023***

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

i) Lengo la makusanyo kwa Mafungu yote ya Wizara hii limeongezeka kwa **asilimia 2.9** ikilinganishwa na lengo la Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha.

ii) Fungu 38 (Ngome) linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha **asilimia 25** Sawa na Mwaka wa fedha 2021/2022.

iii) Fungu 39 (JKT) linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha **asilimia 75** ambapo Mwaka 2021/2022 lilitegemewa kwa asilimia 72.7

iv) Fungu 57 (Wizara) linategemewa kwa makusanyo kwa kiasi cha asilimia 1 wakati Mwaka 2021/2022 lilitegemewa kwa asilimia 1.4 Hata hivyo, kiasi hicho cha Makadirio ya Makusanyo kwa Fungu 57 kinalingana na Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia Maoni ya Kamati kuhusu lengo la ukusanyaji wa Mapato kwa kuzingatia uhalisia wa makusanyo yanayopatikana. Hata hivyo, kwa mara nyingine, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa uhalisia wa makusanyo kwa ajili ya Fungu 57 uangaliwe upya.

## 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya kamati yalibainisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa Mafungu yote matatu ni Shilingi **2,712,787,404,997.00 kati** ya fedha hizo shilingi **2,482,454,233,997.00 sawa** na asilimia 91.5 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **230,333,171,000 sawa na asilimia 8.49** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi mantiki ya Masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma (Items), Vifungu (Subvotes) na Mafungu (Votes) yote ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022.
Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

a) Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 imeongezeka kwa Shilingi **354,092,418,997** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Tofauti hiyo ni ongezeko la asilimia 15. Kamati inaipongeza

Serikali kwa kuzingatia ushauri wake wa mara kwa mara wa kuongeza kiwango cha Bajeti ya Wizara hii na vyombo vyake vyote inavyovisimamia.

b) Kiasi cha fedha kinachoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kimeongezeka kwa Shilingi 53,754,747,000 ambayo ni sawa na asilimia 30.4 ikilinganishwa na kiwango kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Fedha hizi zimeongezeka katika Fungu 38 kwa asilimia 73, Fungu 39 kwa asilimia 249.14 na Fungu 57 kwa asilimia 14.29

c) Kati ya Shilingi **230,333,161,475.00** zinazoombwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za Maendeleo, asilimia 24.47 ni kwa ajili ya Fungu 38- Ngome, asilimia 6.06 ni kwa ajili ya Fungu 39- JKT na asilimia 69.46 ni kwa ajili ya Fungu 57- Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa Mwaka ujao wa Fedha.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri nitakaoutoa. Naomba kubainisha maoni hayo kama ifuatavyo:-

### 5.1 Maoni ya Kamati

(i) Upungufu wa watumishi katika Mashirika ya MZINGA na NYUMBU usipoendelea kufanyiwa kazi na Serikali, utaathiri utekelezaji wa majukumu ya Mashirika hayo na kupunguza tija iliyokusudiwa.

(ii) Kuwezesha inavyostahili utekelezaji wa mradi wa kilimo cha umwagiliaji katika eneo la Chita, ni jambo la kimkakati litakaloongeza uhakika na upatikanaji wa chakula.

(iii) Kukarabati nyumba za makazi ya wanajeshi ni jambo linalochangia kufanikisha azma ya Serikali kuboresha makazi ya Wanajeshi. Aidha, mahitaji ya kibajeti kwa ajili ya ukarabati yanafaa kutimizwa inavyotakiwa.

(iv) Mantiki ya Msajili wa Hazina kukabidhi shamba la Mngeta *(Kilombero Plantation Ltd)* lenye ukubwa wa ekari 14,545 kwa SUMAJKT, inaweza kupatikana iwapo changamoto za uchakavu wa mitambo, miundombinu na ukosefu wa mtaji kwa SUMA JKT zitatatuliwa.

(v) Uzingatiaji wa ushauri wa Kamati ya Bunge kuhusu Sera ya Ulinzi wa Taifa kwa vipindi tofauti umefikia hatua ya kuhitaji kuwekwa katika utekelezaji. Aidha, kupokewa kwa maoni ya

serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wadau wengine muhimu kama ilivyoripotiwa katika Kamati, ni jambo la maana iwapo utekelezaji utaanza.

(vi) Juhudi za Serikali kuimarisha Mipaka yetu ili kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi zinastahili kuendelezwa. Aidha, ili kuendelea kudhibiti mianya ya mipaka inayoweza kutumiwa isivyostahili, Serikali inapaswa kuboresha uratibu wa jambo hilo.

(vii) Kukosekana kwa hati za Maeneo yanayomilikiwa na Wizara ya Ulinzi ni jambo linalochangia kuwavutia baadhi ya wananchi kuvamia maeneo hayo na baadaye kuibuka kwa migogoro ya umiliki.

## 5.2 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa maoni hayo, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 57 (Wizara) kwa mtiririko uliopangwa. Aidha, Serikali itoe kwa ukamilifu fedha zote za maendeleo ambazo bado hazijatolewa kwa Fungu 38 (Ngome) na Fungu 39 (JKT) ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

(ii) Jeshi la Wananchi liandae na kutekeleza mkakati wa muda mrefu wa kupeleka Askari wenye utaalamu unaohitajika katika Mashirika ya NYUMBU na MZINGA. Kufanya hivyo itapunguza

upungufu wa rasilimaliwatu kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika uzalishaji.

(iii) Serikali kupitia Wizara ya Fedha itenge Shilingi 9.5 bilioni zinazohitajika kwa ajili ya kumalizia miundombinu ya umwagiliaji na kusawazisha *(leveling)* shamba la Jeshi la Chita kwa ekari 2500. Aidha zitolewe fedha za kununua mitambo na mashine za kisasa za kilimo kwa kuanzia mwaka wa Fedha 2022/2023.

(iv) Serikali kupitia Wizara ya Fedha iandae utaratibu mahsusi utakaowezesha upatikanaji wa fedha kwa aijili ya kufanya ukarabati wa nyumba za makazi ya Wanajeshi.

(v) Serikali itoe ruzuku kwa SUMAJKT ili kuendeleza kilimo cha kisasa katika shamba la Mngeta na kuweza kuzalisha mazao ya kutosha.

(vi) Serikali ikamilishe upatikanaji wa Sera ya Taifa ya Ulinzi (*The National Defence Policy*) kwa umuhimu wake kwa taiafa kama ambavyo imekuwa ikishauriwa vipindi tofauti tangu Bunge la Tisa.

(vii) Serikali ichukue hatua madhubuti za kuendelea kuimarisha miundombinu ya kiulinzi na kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi katika mipaka yetu pamoja na mwambao wa Bahari ya Hindi.

(viii) Serikali itoe kiasi cha fedha kitakachotengwa kwa ajili ya Mashirika ya kimkakati ya NYUMBU na MZINGA kadri zitakavyoidhinishwa na Bunge na kulingana na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

(ix) Uandaliwe mkakati maalum unaotekelezeka wa kupima na kupata Hati za maeneo yote ya Wizara hii ambayo hayajapimwa.

(x) Serikali ikamilishe mchakato wa kuruhusu Jeshi kuwa na Bounded Warehouse yake.

(xi) Serikali iendelee kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili kibajeti miradi ya wizara ili kupata tija iliyokusudiwa kwa maslahi mapana ya Taifa.

(xii) Wizara iendelee kutekeleza Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika Bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2019/2020, 2020/2021 na 2021/2022.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard):

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb | - | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Vicent Paul Mbogo, Mb | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb | | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Cosato David Chumi, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Alexander Pastory Mnyeti, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb | | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Ali Juma Mohammed, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb- | | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Stagomena L. Tax kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Faraji Mnyepe pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J Mwihambi, ndc kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Omary Magwinza na Bi. Victoria Mizengo na wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**Vita Rashid Kawawa, Mb**

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

Mei, 2022

***KIAMBATISHO NA. 1***

**UTELEKEZAJI WA MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA (NUU) KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2021/2022**

---

***(i) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 39- JKT kwa mtiririko uliopangwa. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2021, Fungu hili lilikuwa halijapokea fedha zozote kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Maendeleo. Aidha, Serikali itoe kwa ukamilifu fedha zote za maendeleo ambazo bado hazijatolewa kwa Fungu 38 (NGOME) na 31 Fungu 57 (Wizara) ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.***

Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Fungu 39 – JKT limeidhinishiwa **Shilingi 4,000,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 limepokea **Shilingi 3,501,349,288.00**.

Aidha, Fungu 57 – Wizara na Fungu 38 - NGOME yamepokea **Shilingi 83,803,992,017.65** kati ya **Shilingi 150,000,000,000.00** na **Shilingi 9,694,160,292.32** kati ya **Shilingi 10,000,000,000.00** mtawalia katika kipindi husika. Ni matumaini ya Wizara kuwa Serikali itatoa fedha zilizobaki hadi kufikia mwezi Juni, 2021. Tunaishukuru Serikali kwa kuendelea kuiwezesha Wizara ya Ulinzi na JKT na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake.

- ***(ii)*** ***Serikali itoe fedha zote zilizotengwa katika mwaka 2020/2021 kwa ajili ya kukarabati nyumba za makazi ya wanajeshi. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2021, hakuna fedha zozote zilizotolewa kwa ajili ya shughuli hiyo.***

  Wizara ya Ulinzi na JKT inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za makazi ya wanajeshi.

- ***(iii)*** ***Serikali ikamilishe na kuanza utekelezaji wa Mpango wake wa miaka kumi (2021/22-2030/31) wa kuliimarisha Shirika la NYUMBU kuweza kukabiliana na changamoto ya uchakavu wa mitambo na teknolojia iliyopitwa na wakati. Hii italiwezesha Shirika hilo kutekeleza shughuli zake za msingi kwa ufanisi zaidi na hivyo kuokoa fedha nyingi za Serikali.***

  - Wizara imekamilisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Kumi (2021/22 – 2030/31) wa Kuliimarisha Shirika la Tanzania Automotive Technology Centre (TATC) kwa kupitishwa katika ngazi mbalimbali za maamuzi ikiwemo IMTC na Baraza la Mawaziri. Aidha, utekelezaji wa Mpango huo unatarajiwa kuanza katika Mwaka wa Fedha 2021/2022.

  - Kamati inapongeza Serikali kwa kuongeza makadirio ya Bajeti ya Mashirika ya NYUMBU na MZINGA kutoka **Shilingi bilioni 7.5** hadi **bilioni 9** na **Shilingi bilioni 4** hadi **bilioni 5.5** mtawalia kwa mwaka 2021/22. Aidha inategemewa Serikali itatoa fedha hizo kwa kadri

zitakavyoidhinishwa na Bunge na kulingana na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

***(iv) Serikali ihakikishe kuwa Awamu ya Pili ya Huduma za Bima ya Afya (Oktoba 2021 hadi 2026) inatekelezwe kama ilivyopangwa ili kuwezesha Wanajeshi kupata huduma za afya katika Hospitali za Jeshi, Serikali, Hospitali Binafsi pamoja na Mashirika ya Dini.***

Wizara imepokea maoni ya kamati na imejipanga kuhakikisha Awamu ya Pili ya Huduma za Bima ya Afya kwa Wanajeshi ambayo inatarajia kuanza mwezi Oktoba, 2021 hadi Septemba, 2026 inatekelezwa. Awamu hii itahusisha huduma za afya katika Hospitali za Serikali, Binafsi pamoja na Mashirika ya Dini.

***(v) Serikali ikamilishe upatikanaji wa Sera ya Ulinzi ambayo Kamati imekuwa ikishauri kwa vipindi tofauti tangu Bunge la Tisa. Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilieleza kuwa tayari maoni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yameshapokelewa na taratibu nyingine za kuwasilisha katika Baraza la Mawaziri zinaendelea.***

Wizara imepokea maoni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wadau wengine muhimu na inaendelea kuyafanyia kazi. Aidha, ni mpango wa Wizara kuhakikisha kuwa Sera hiyo inakamilika mapema iwezekanavyo.

***(vi) Serikali iendelee kuimarisha miundombinu ya kiulinzi iliyopo katika mipaka yote ya Nchi ikiwa ni pamoja na barabara, alama za mipaka na mengineyo.***

Suala la uimarishaji wa miundombinu ya kiulinzi katika mipaka ya nchi ikiwa ni pamoja na barabara za ulinzi, alama za mipaka na mengineyo ni mtambuka, likihusisha Wizara nyingine ikiwemo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Wizara ya Ulinzi na JKT kwa kushirikiana na wadau hao itaendelea kuimarisha miundombinu hiyo ikishirikiana na nchi tunazopakana nazo.

***(vii) Serikali iweke utaratibu wa kutoa fidia badala ya kulipa kodi ya pango katika maeneo ya Wananchi ambayo yametwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa minara ya Mawasiliano Salama Jeshini. Kwa kufanya hivyo Serikali itamiliki maeneo hayo lakini pia itaokoa fedha nyingi ambazo zingeendelea kulipwa kama kodi ya pango.***

Wizara ilikwishaongea na wamiliki wa maeneo ilikojengwa minara. Baadhi waliridhia maeneo yao yatumike bila kulipiwa kodi ya pango la ardhi. Wengine walitaka walipwe fidia ya ardhi ili ardhi hizo zitwaliwe na kumilikiwa na Wizara ya Ulinzi na JKT. Wizara kwa sasa imekwishaunda timu zitakazokwenda mikoani kufanya uthamini wa maeneo ili wahusika walipwe fidia.

***(viii) Serikali ifanye tathmini ya mahitaji halisi ya nyumba za makazi kwa Wanajeshi itakayojumuisha nyumba 3,936 zilizobaki katika mradi wa Nyumba 10,000 na kutenga***

***bajeti ya utekelezaji wake ili kupunguza changamoto ya nyumba za makazi kwa Wanajeshi.***

Tathimini ya mahitaji halisi ya nyumba za makazi ya Wanajeshi imeshaanza na inatarajiwa kukamilika katika Mwaka wa Fedha 2021/2022.

***(ix) Serikali ihakikishe masharti ya mikopo hiyo yanaruhusu Serikali kuchagua Mshauri elekezi na Mkandarasi wa kujenga nyumba hizo ili kuhakikisha zinakuwa na viwango vya ubora unaotakiwa.***

Maoni ya kamati yamepokelewa. Wizara itajitahidi kuhakikisha kuwa masharti ya mikopo ya ujenzi yanaruhusu Serikali kumchagua Mkandarasi na Mshauri Elekezi wa kutekeleza miradi inayokusudiwa kwa ufanisi.

***(x) Serikali itoe fedha hizo kwa kadri zitakavyoidhinishwa na Bunge na kulingana na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ili kuwezesha tija inayokusudiwa.***

Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha bajeti inayoidhinishwa inatolewa kulingana na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

***(xi) Serikali ikamilishe Mpango wake wa kuwapatia wahitimu wote wa kidato cha Sita mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria. Aidha, ili kufanikisha mpango huo, Serikali itenge na kutoa fedha kwa ajili ya kuongeza Makambi na kuboresha miundombinu ya Makambi yaliyopo.***

Wizara imeandaa mpango utakaowezesha kuchukua Vijana wote wanaohitimu kidato cha sita kupata mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria. Mpango huo umeanza kwa kutathmini uwezo wa makambi yaliyopo pamoja na kushirikisha wadau muhimu wakiwemo Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) na Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu (TCU) ili kubaini muda sahihi wa mafunzo. Pamoja na mpango huo Wizara ya Ulinzi na JKT inategemea kuongeza idadi ya Vijana wa Mujibu wa Sheria kutoka 21,000 mwaka 2020/2021 hadi kufikia vijana 35,000 kwa mwaka 2021/2022.

JKT imepokea fedha za maendeleo kiasi cha **Shilingi 3,501,349,288.00** katika mwaka 2020/21. Fedha hizo zimetumika kukarabati na kujenga Makambi ya JKT. Aidha, Wizara itaendelea kuongeza bajeti ya kuboresha miundombinu ya Makambi yaliyopo ili yaweze kuongeza idadi ya Vijana wa Mujibu wa Sheria wanaochukuliwa.

***(xii) Serikali ikamilishe kwa haraka Mpango wa kuwawezesha vijana wanaojitolea kwa ajili ya mafunzo ya JKT kupata mitaji kwa kushirikisha Sekta na Taasisi nyingine. Wakati wa majadiliano na Wizara hii Kamati ilielezwa kuwa Utekelezaji wa Mpango huu unasimamiwa na Wizara ya Ulinzi na JKT kwa kushirikisha Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Kazi na Ajira, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.***

Jukumu la msingi la Jeshi la Kujenga Taifa ni kutoa mafunzo na malezi ya Vijana ili kuwajengea uzalendo na

ukakamavu. Katika kutekeleza jukumu hilo, Vijana hufundishwa stadi za maisha zitakazowawezesha kujiajiri pindi wanapomaliza mafunzo.  Vijana hupata Stadi hizo za maisha kupitia shughuli mbalimbali za JKT zikiwemo kilimo, mifugo, viwanda na kupitia miradi mbalimbali ya ujenzi zinazofanywa na JKT.

Kupitia vyuo mbalimbali vya ufundi stadi vilivyopo JKT Vijana hupatiwa mafunzo ya ufundi stadi ikiwemo useremala, ushonaji, ufundi mchundo, ufundi magari na umeme. Mafunzo haya huwapa ujuzi vijana kuweza kujiajiri wanapomaliza mafunzo. Aidha, Vijana hupatiwa vyeti vinavyotambuliwa na VETA na NACTE ili ujuzi wao uweze kutambuliwa baada ya kumaliza mafunzo. Wizara imefanya mazungumzo na Taasisi zingine zikiwemo Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu Ajira, Kazi, Vijana na wenye Ulemavu kwa lengo la kuwasaidia vijana kuanzisha miradi na kupata mitaji.